**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**Juni, 2023**

**Dodoma**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Namba za Simu**

**Mkuu wa Shule 0717653199/0656471414**

**Makamu Mkuu wa Shule 0714019535**

**Matron/Patron0653347704/0755177704**

**Shule ya Sekondari KWIRO**

**S.L.P 06 MAHENGE/ULANGA**

**Tarehe .....................…………….**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**

**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KWIRO HALMASHAURI YA WILAYA YA ULANGA MKOA MOROGORO MWAKA 2023/2024**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2023/2024 na atasoma tahasusi ya ………….

Shule ya Sekondari Kwiro ipo umbali wa Kilometa 2 Magharibi mwa Mji wa Mahenge. Usafiri wa basi kutoka mjini Morogoro unapatikana katika kituo cha mabasi Msavu Morogoro/Mbezi Dar Es Salaam Nauli ni Shilingi **tsh 25,000** kwa Morogoro na **tsh 30,000** kwa Dar Es Salaam. Kampuni Za mabasi ya **KIDINILO/MBEKENYERA/AL-SAEDY** zinatoa huduma ya safari za moja kwa moja kutoka kwenye vituo vya basi mpaka Mahenge. Kutoka kituo cha mabasi Mahenge kwa pikipiki ni Shilingi tsh 2000/= tu hadi shuleni.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe **13/08/2023** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **13/08/2023** Mwisho wa kuripoti ni tarehe **27/08/2023**

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

i. Sare ya shule hii ni Suruali mbili za rangi ya Dark Blue zenye marinda ,zisiwe za kubana (model) au mshono wa jinsi.

ii. Mashati mawili meupe ya mikono mirefu

iii. Sare ya Michezo ni kwa shule hii ni fulana mbili na bukta mbili kwa mchanganuo ufuatao

A) PCB Rangi ya bluu

b) CBG, Rangi ya manjano

c) PCM, Rangi nyekundu

d) EGM, Rangi nyeupe

e) HGE, Rangi ya kijani

f) HGL, Rangi ya damu ya mzee

g) HGK, Rangi ya kijivu

iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;

v. Soksi jozi mbili nyeusi

vi. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;

vii. Sweta mbili za rangi ya dark blue (zinapatikana kwenye duka la shule)

viii. Nguo za kushindia (*shamba dress*) ni Truck suit mbili za rangi ya dark blue

ix. Tai mbili za mistari ya pundamilia yenye rangi ya dark blue na rangi nyeupe iliyolala (zinapatikana kwenye duka ka shule)

x. Tisheti (T-shirt) mbili za rangi ya dark blue zenye kola (maarufu form six) zinapatikana kwenye duka la shule

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari kumi na mbili (12) counter books za quire 3 au 4

ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;

iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha iambatishwe*);

iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;

v. Scientific Calculator;

vi. Godoro la sponji la ukubwa wa futi mbili na nusu kwa sita unashauriwa kununua maduka karibu na shule

vii. Mashuka Jozi 2 za rangi ya light blue, blanket 1, foronya ya godoro 1 ya rangi ya light blue, chandarua 1

viii. Nguo za ndani za kutosha;

ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe vyote vya bati)

x. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;

xi. Kwanja 1 lenye mpini wa mbao, jembe 1 na ufagio laini kwa michepuo ya HGL, HGK NA EGM, Panga 1, mifagio miwili (2) hard broom na squeezer kwa

michepuo ya PCM,PCB na CBG, chepe 1 na ufagio wa chelewa wa nje kwa mchepuo wa HGE.

xii. Kila mwanafunzi anaombwa kuja na flat file mbili, moja kwa ajili ya kutunza mazoezi na miotihani yake na moja titakabidhiwa ofisi ya taaluma kwa ajili ya kumbukumbuku za mwanafunzi kwa muda wote atakao kuwa anasoma hapa shuleni

ANGALIZO: **Kuepukana na usumbufu unaojitokeza sambamba na kuibiwa wazazi mnashauriwa kununua vifaa vyote maeneo ya shule kwani huduma za kifedha zinapatikana shuleni**

### 2.3 Michango mbalimbali ya shule

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Michango yote ilipwe kwenye akaunti ya shule kwa akaunti namba **21901000019 NMB kwa jina la KWIRO SECONDARY REVENUE COLLECTION** (Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye paying slip ya bank)

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;

ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;

iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);

iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;

v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uwanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kuwa na nywele ndefu au kusuka rasta
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kusababisha mimba;
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

xviii. Kutohudhuria vipindi vya dini ambavyo vipo kwa mujibu wa sheria na kanuni za shule

xix. Kukutwa na kitu chochote hatarishi kinachoweza kusababisha moto bwenini kama vifaa vya umeme, mafuta ya taa, petrol au spirit

xx. Kukutwa bwenini wakati wa vipindi vya darasani mchana au usiku (wakati wa maandilizi) bila kibali cha mwalimu wa malezi

xxi. Kuwa nje ya uzio wa shule bila ruhusa

**MUHIMU**

**Mwanafunzi haruhusiwi kuja na redio, pasi ya umeme au kifaa kingine chochote kinachotumia umeme**

**3. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;

ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;

iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na

iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

v. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KWIRO SEKONDARI**

**Saini ya Mkuu wa Shule ………………………………………**

**Jina la Mkuu wa Shule JOHN A. KASHAMBA**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0717653199**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0714019535**
- **Mwandamizi Taaluma 0656471414**
- **Mwandamizi Malezi 0653347704/0652971882**

## STUDENT MEDICAL CERTIFICATE

To be completed by the Government Medical Officer and return to the Headmaster of Kwiro Secondary School BOX 06 Mahenge/Ulanga
Date……………………………

**To the medical officer**
………………………………………..
……………………………………………….
…………………………………………………
Re………………………………………………………………..
Please examine the student mentioned above and comment on his health by responding to the following items. Kindly put a tick or cross in front of either Yes or No
Headmaster
1. Does the student have the problem in connection with
a) Sight?..........No ( ) Yes ( )
If Yes state and recommend……………………………………………………………………………
b) Hearing?............ No ( ) Yes ( )
If Yes state and recommend……………………………………………………………
c) Speech?............. No ( ) Yes ( )
If Yes state and recommend…………………………………………………………………………
TB? .......... No ( ) Yes ( )
If Yes state and recommend………………………………………………………………………………………
BP?......... No ( ) Yes ( )
If Yes state and recommend……………………………………………………………………………………
Any other disability?………… No ( ) Yes ( )
if Yes state and recommend…………………………………………………………………………………………………………………………………
What is your recommendation on the said student medical fit for studying at this school
……………………………………………………………………………………………
………………………..………………………………………………………………………
…………………………………………………..

## UTHIBITISHO WA MZAZI/MLEZI

Mimi Mzazi/Mlezi wa ………………………………………………………………………
Nitahakikisha mwanangu anafuata sheria, kanauni na taratibu zote kama ilivyoagizwa kwenye barua ya kujiunga na shule hii na kutimiza michango yote kwa wakati na kwa kipindi chote ambacho atasoma hapo shuleni
Jina la Mzazi/Mlezi…………………………………………………………………………

Sahihi……………………………………………….
Tarehe……………………………………………

***NB: Kabidhi fomu hii wakati wa kuripoti au usajili***

## Yah: KUTAMBUA UWEPO WA SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE

Mimi……………………………………………………………………………wa kidato …………………..mchepuo wa…………………..ninaahidi kufuata taratibu zote kama nilivyoelekezwa na Uongozi wa shule pamoja na barua ya kujiunga niliyopewa. Nikikiuka nichukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria,kanuni na taratibu za shule ichukue

Sahihi……………………………………….
Tarehe…………………………………….

# STUDENT MEDICAL CERTIFICATE

To be completed by the Government Medical Officer and return to the Headmaster of Kwiro Secondary School BOX 06 Mahenge/Ulanga
Date……………………………

**To the medical officer**
………………………………………..
…………………………………………….
………………………………………………
Re……………………………………………………………………..
Please examine the student mentioned above and comment on his health by responding to the following items. Kindly put a tick or cross in front of either Yes or No
Headmaster
1. Does the student have the problem in connection with
a) Sight?..........No ( ) Yes ( )
If Yes state and recommend……………………………………………………………………………
b) Hearing?............ No ( ) Yes ( )
If Yes state and recommend………………………………………………………………
c) Speech?............. No ( ) Yes ( )
If Yes state and recommend…………………………………………………………………
TB? .......... No ( ) Yes ( )
If Yes state and recommend……………………………………………………………………………
…………
BP?......... No ( ) Yes ( )
If Yes state and recommend……………………………………………………………………………
………
Any other disability?………… No ( ) Yes ( )
if Yes state and recommend……………………………………………………………………………
……………………………………………
What is your recommendation on the said student medical fit for studying at this school
…………………………………………………………………………………………………
………………………..………………………………………………………………………
…………………………………………………..

## UTHIBITISHO WA MZAZI/MLEZI

Mimi Mzazi/Mlezi wa ………………………………………………………………………… Nitahakikisha mwanangu anafuata sheria, kanauni na taratibu zote kama ilivyoagizwa kwenye barua ya kujiunga na shule hii na kutimiza michango yote kwa wakati na kwa kipindi chote ambacho atasoma hapo shuleni
Jina la Mzazi/Mlezi…………………………………………………………………………

Sahihi……………………………………………….
Tarehe……………………………………………

***NB: Kabidhi fomu hii wakati wa kuripoti au usajili***

## Yah: KUTAMBUA UWEPO WA SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE

Mimi…………………………………………………………………………………wa kidato …………………..mchepuo wa…………………..ninaahidi kufuata taratibu zote kama nilivyoelekezwa na Uongozi wa shule pamoja na barua ya kujiunga niliyopewa. Nikikiuka nichukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria,kanuni na taratibu za shule ichukue

Sahihi……………………………………….
Tarehe…………………………………….